



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Wednesday, 24th April, 2024

Third Assembly – Third Session
TWENTY EIGHTH SITTING

*[The County Assembly met at 2:33p.m. at the County Assembly Buildings]
[The Temporary Speaker (Honourable Frankline Makanga) in the Chair]*

PRAYERS

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Let us be seated Honourable Members.
Yes Clerk? Next order please.

PAPER

COUNTY GOVERNMENT OF MOMBASA, MOMBASA COUNTY CONSOLIDATED REVOLVING FUND,
QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENT FOR THE QUARTER ENDED DECEMBER 31st, 2023

Yes, Honourable Bernard Ogutu, please lay the Paper.

[Paper laid]

Thank you. Honourable Members, the Report on quarterly Report and Financial Statement for the quarter ended December 31st, 2023 on the Mombasa County Consolidated Revolving Fund, stands committed to the Committee on Finance, Budget and Appropriation for consideration. Yes Clerk?

STATEMENTS

STALLED CONSTRUCTION OF MAJAONI NEW LIFE ROAD AND KASHANI ROAD

Yes, Honourable Patrick Mbele MCA Bamburi Ward?

[Silence]

There being no representation, the matter to be taken back to the County Assembly House Business Committee. Yes, Clerk next order please?

REQUEST FOR STATEMENT BY MEMBER OF COUNTY ASSEMBLY (MCA) FREE TOWN HONOURABLE
MARIAM BAIMU ON MOGOKAA, MIRAA AND OTHER SUBSTANCE CONTROL IN THE COUNTY

Yes, Honourable Maryam Baimu MCA Free Town, can you make a Statement.

Hon. Baimu: Thank you Mr. Speaker Sir. I wish to put a statement on Mogokaa, Miraa and other Substance Control in the County of Mombasa. Mr. Speaker Sir, I seek pursuant to Standing Order 41(2)(c) to request a statement from the Chairperson, Committee on Health Services on the pressing issues of Mogokaa, Miraa and other drugs substance abuse within the County. It is important that we acknowledge the detrimental effects this problem has on health, safety and overall well-being of our community. Honourable Speaker, as representatives of the people, it is our duty to address this matter with urgency and determination. We must inquire into the plans and action of the County government regarding the mitigation of Mogokaa, Miraa and other drugs and substance abuse. Honourable Speaker Sir, in his response, the Chairperson should report on;

1. What measures the County government has in place to combat this issue effectively.
 2. What measures are in place in as far as prevention, treatment and rehabilitation is concerned
- Thank you, Mr. Speaker Sir.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Thank you Honourable Maryam Baimu for the request for the Statement and through the powers vested in me as the Chair of this sitting, I would like to open this conversation to any other Member who is in the House to react on the matter raised concerning Mogokaa, Miraa and other drug substance abuse within our County. If anyone has any remarks, please you are free to do so before we give an opportunity to the Chair, Health Committee to respond. So, Honourable Pamela Ojala please can you make your reactions?

Hon. Ojala: Ahsante Mheshimiwa Spika kunipatia fursa hii. Mheshimiwa Spika, vile sisi sote tunajua *Mogokaa* imeathiri watoto wetu sana, umefanya watoto wetu wanakosa kusoma, imefanya watoto wetu wanakatakata watu na mapanga, sasa ni muhimu sana kushughulikiwa haya mambo ya *Mogokaa* ili tuweze kuwa na usalama. Mheshimiwa Spika, hata sisi kina mama pale majumbani tumekosa amani na wanaume wetu kwa sababu huu *Mogokaa* mwanamme atakaa masaa 12 akichonga. Na mimi naomba kama Mheshimiwa Spika haya mambo ya *Mogokaa* yaweze kushughulikiwa na sisi ili tuweze kuwa na amani katika majumba yetu. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Thank you so much Honourable Ojala. Yes, Honourable Leila Nyache, Member of County Assembly for Kipevu Ward please make your reactions?

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kuniona nami niweze kutia sauti yangu pia. Mheshimiwa Spika, kusema kweli huu *Mogokaa* umeathiri ama umeharibu vijana wetu na hata wazee wa makamu pia wenye ambao kwamba wanatumia *Mogokaa*; wengine hata kazi pia hawa vijana wetu hawataki kazi kwa sababu wakishaambua ule *Mogokaa*, wana ambua kucha ule *Mogokaa* na asubuhi hawezi kuamka, kuamka kwake basi ni saa tisa haya mtoto huyo ataenda kazini kweli! Hataweza kwenda! Kwa hivyo kama vile mwenzangu ametangulia kusema huo *Mogokaa* uweze kupigwa marufuku kabisa, utolewe na pia hata kama vile tumesema katika sheria bei ya kulipa Kaunti iwe juu ipandishwe kabisa kwa sababu ukipandishwa hivyo ndio labda utapungua watapunguza kuuza na hata hawa wazee wetu ambao ni watu wazima ovyo pia nao hukaa maskani na kuweza kula *Mogokaa* na wana familia zao hawafikirii chochote pia wao wametelekeza familia zao kwa ajili ya *Mogokaa*.

Kwa hivyo mimi naungana na wenzangu niweze kupinga hili jambo la *Mogokaa* na pia liweze kuwekwa katika sheria kali katika Bunge la Kaunti yetu. Ahsante.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Thank you so much Honourable Leila Nyache. Yes, Honourable Mwaka Muludonda, please make your reactions?

Hon. Muludonda: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kujadili jambo la kuhusiana na *Mogokaa*. Kwa kusema kweli *Mogokaa* ni kitu ambacho ni sumu kubwa sana; imeathiri jamii hususan vijana wetu kwa sababu vijana wakila *Mogokaa* hawana hisia hata za kupatia wasichana wao... wanajihisi wakitafuna pale wako na mrembo tu kwa kichwa chake ndio wakati unamalizika masiku yanazidi kusonga...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Mheshimiwa Mwaka hisia kupatia msichana labda ufafanue kwa sababu ni Jumba la sheria...

[Interruption]

Hon. Muludonda: Hana hamu ya mwanamke...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Hamu ya aina gani?

Hon. Muludonda: Hamu ya ku...

[Laughter]

Hamu ya tendo la ngono; ya kujamiana baina ya mume na mke!

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Ahsante Mheshimiwa Mwaka.

Hon. Muludonda: Kijana yule atakaa maskani; la pili hataki mwanamke ambapo natarajia kama mimi mama Mwaka nataka kuitwa nyanya na kijana yeye atakuwa anakula *Mogokaa* hawezi kupata mwanamke akapata mtoto ili tukaongeza jamii. Kwa hiyo mimi napinga jambo hili na nalikemea liweze kutiliwa nguvu ikiwezekana hata tuseme tunapiga marufuku kabisa na kama pengine tutakuwa tumeshindwa na nguvu hizo basi tuweke kiwango cha hali ya juu sana mpaka kiasi cha kwamba hawataweza kununua ama kupata *Mogokaa* kwa sababu *Mogokaa* ni bei nafuu. Hususan kama saa hizi ni wakati wa mvua *Mogokaa* hata shilingi 20 labda anapewa, watoto wa shule pia wanakula *Mogokaa*, watoto wadogo! Tulipata nafasi ya kutembelea shule hapa Likoni tukapata Mwalimu ana sema ikifikia asubuhi mpaka chakula cha mchana moto ni moto darasani ikifikia wakati wa chakula cha mchana mtoto anamtolea Mwalimu macho hajui aseme nini huku anatafuna *Mogokaa*. Kwa hiyo mimi nasema nakemea na natilia nguvu Mswada huu uweze kutuokoa vijana wetu na jamii kwa jumla Mombasa na Kenya nzima tuweze kupata usaidizi wa jambo hili wa hii sumu inaitwa *Mogokaa*. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Ahsante sana Mheshimiwa Mwaka kwa changizo yako kwa sababu ya Rekodi za Bunge hili ieleweke kwamba ni Ombi la Taarifa sio hoja. Kwa hivyo naomba ambayo Mheshimiwa ameitisha ambapo Mwenyekiti wa Kamati ya Afya atafaa kujibu, kwa hivyo ahsante. Mheshimiwa Nusura Mwinyi Muwakilishi Wadi eneo la Mtongwe upande wa Feri.

Hon. Nusura Mwinyi: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nataka kupongeza sana hii Taarifa ya *Mogokaa*. La pili, nataka niseme ndani ya Bunge hili, *Mogokaa* umetuathiri sana watoto wetu; umeathiri sana watoto wetu na si watoto wetu pekee hata pia kuna watu wazima pia wanatumia huu uraibu na saa nyengine ukiwasikiza sana kwanza kwa upande wa wanawake, ukiwauliza kwa nini wanapenda kutumia uraibu huu wengi watakuambia mimi niko *low libido*, sasa wengi wanasema wanatafuta *booster*. Alafu pia kuna vijana wetu nafikiri Mombasa yetu imeathirika zaidi kuliko Kenya nyengine, si ni kweli?! Mombasa tumeathirika zaidi, watoto wetu wamebobeza kwa huu ulaji wa *Mogokaa* na tukiangalia mimi kwa mtazamo wangu, kama hapa Mombasa kwetu vijana kuanzia miaka kumi, miaka tisa wako ndani ya uraibu wa *Mogokaa*! Labda tukija miaka hamsini ijayo Mombasa watu watakuwa wamepungua, idadi ya watu itakuwa ni kidogo na ni kwa sababu ya huu *Mogokaa*! Na nataka kusema watoto wetu wakila *Mogokaa* wengi huwa hawasababishi na nasema hivyo kwa sababu watoto wetu sasa hivi hawaoi, watoto wetu hawataki wasichana, watoto wetu hawatongozi! *Mogokaa* unawafanya wanalemaa, *Mogokaa* unawafanya wanakosa nguvu za kiume! Kwa hivyo mimi moja kwa moja niko pamoja na yule aliyeleta Taarifa hii ili kupinga *Mogokaa*; kwa wale ambao ni waraibu watatusamehe kwa sababu hatuwezi kukubali kuishi na kitu ambacho ni sumu kweli. Kwa hayo mengi ama machache nasema ahsante sana Mheshimiwa Spika tunapinga sana swala hili la *Mogokaa*.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Ahsante sana Mheshimiwa Nusura Mwinyi, na Mheshimiwa Mohammed Hamid. Mheshimiwa Mohammed Hamid hapa kuna hoja ambayo imeletwa ama ombi la kuweza kupata majibu kuhusiana na utumizi ama athari za *Miraa* na *Mogokaa*, changizo lako?

Hon. Mohammed Hamid: Ahsante Ndugu Spika kwa fursa hii ya kunipa mimi kuchangia. Ningelipenda hoja hii... lazima tuliangalie jambo hili kwa kina; kuna waraibu wa *Mogokaa* na *Miraa*, hizi ni biashara ambazo zimekuwa ndani ya miji yetu mikubwa ya Kenya kwa muda mrefu sana. Mimi ombi langu ni moja tu, hapo zamani kulikuwa na biashara ya *Miraa* lakini tatizo hili tulikuwa hakuna, kwa nini sasa tuna tatizo hili? Lazima sisi kama viongozi tujiulize tatizo hili limetoka wapi, limeanza wapi! Hapo awali biashara kama hizi za *Miraa* zilikuwako haziko kila sehemu, zilikuwa zinafanywa lakini sehemu fulani peke yake. Ukitaka *Miraa* mpaka uende Mwembe Tayari lakini sisi kuwacha biashara hii bila ku *regulate* ama bila kuweka sheria ya Mahakama za kusimamia biashara hii ndio imeleta madhara yote haya. Kwa hivyo nafikiria sisi kama Bunge la Kaunti ama kama wanasheria, ni tubuni sheria ambazo zitaweza kufanya biashara hizi zifanyike lakini kwa maeneo fulani ambapo sisi kama serikali tunajua biashara hizi zinafanyika sehemu fulani peke yake na sivyo zinavyo fanyika sasa hivi ya kuwa biashara hizi watu wanauza *Mogokaa* ndani ya majumba yao hata saa nane za usiku, samahani kutumia lugha hii, ikiwa umeketikiwa pia waweza kupata kwenye majumba yauzwa. Kwa hivyo ni sisi tubuni sheria ya namna gani hizi biashara zitakavyo fanywa hatuwezi kusema kuwa tutazipinga kabisa kwa sababu ni biashara za watu wetu wenyewe wakulima wa Kenya. Kwa hivyo mimi ombi langu ni sisi tubuni sheria ambazo zitakazo weza kusimamia biashara hii ya *Mogokaa*. Ahsante sana Ndugu Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Ahsante sana Mheshimiwa Mohammed Hamid Mwenyekiti wa chama cha Chungwa katika mji wa Mombasa. Mheshimiwa Shuhudia tafadhali fanya changizo lako.

Hon. Shuhudia Abdallah: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa mwenza Mariamu Baimu kwa kuleta hoja hii. Mimi kwa mtazamo wangu naona *Miraa* imeharibu sana vijana na pia kina mama. Kuna kina mama ambao pia wanatumia *Mogokaa* ambao pia wengine wanaacha watoto ama wanatupa watoto kwa sababu ya *Mogokaa*. Kwa hivyo mimi naomba huu *Mogokaa* kama alivyosema Mheshimiwa mwenza uwe una mahali maalum ama mahali ambapo utauzwa utakuwa ni mahali ambapo ni pamoja sio kila mahali utapata pia watoto wa shule saa hii kila mtu ukimuona ana kipakiti chake kana kwamba ni ni pakiti ya chakula kumbe ni kipakiti cha *Mogokaa*. Hivyo basi mimi naomba Mheshimiwa Spika tukae chini sisi kama wanasheria hapa tutunge sheria kali ambayo itakuwa pia mtoto hawezi kununua maanake saa hii tuko rahisi kwa sababu ya mvua pia nasikia ki pakiti sasa hivi ni shilingi kumi; shilingi kumi pia unaweza kupata *Mogokaa*. Kwa hivyo langu ni hilo ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Patrick Mbelle Mwakilishi Wadi ya Bamburi?

Hon. Mbelle: Mheshimiwa Spika jambo ama swala la *Mogokaa* aliomba ombi la kupewa majibu Mheshimiwa wa Frere Town; nafikiri majibu mengine hata sisi wenyewe tuko nayo, kando na kupeleka na kupewa hiyo *professional Report* kutoka kwa idara, moja kwa moja tukianza na watoto wachanga hili jambo linaanza kutoka kwa watoto wachanga mpaka kwa watu wazima. Watoto wachanga ambao wananyonyeshwa maziwa kutoka kwa mama zao wanaotumia *Mogokaa* wengi ukienda katika Hospitali zetu kama Makadara na hospitali zengine utawapata watoto wako na kitu inaitwa *insomnia*. *Insomnia* mtoto chini ya mwaka mmoja halali analia kuanzia asubuhi hadi jioni; muda ukienda mtoto anaweza kuwa na magonjwa ambayo yana athari kubwa katika maisha yako. Kwa hivyo ni kwa mtoto mdogo mamake mwenyewe mzazi wengine wanasema bado ni *booster* nimesikia jambo kama hilo lakini kadri unapofanya ni *booster* lakini mazoea yakizidi mwisho wa siku hata hiyo *booster* inakata kila kitu. Vilevile kwa vijana wenzetu Mheshimiwa Spika leo hii kipakiti cha *Mogokaa* hata kimepungua ile idadi yake bado ni shilingi hamsini ile utapata kijana yule utampata kwa siku moja amekula vipaketi vinne ama vitano, wengine huenda mpaka kumi! Kwa hivyo ile hamsini, hamsini ni shilingi mia tano hivyo huo ni mshahara wa mtu mmoja kwa siku anayefanya kazi.

Kwa hivyo unapata bado vijana wengi wako na vibarua hapa na pale lakini bado wanaishi majumbani kwao anategemea mzazi anakua kero katika jamii. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika kivyovyote vile ukiangalia athari yake inazidi manufaa kwetu sisi kama jamii na alivyosema Mheshimiwa Hamid Mwenyekiti wa chama cha utawala huku Mombasa ni kwamba hii ni biashara kwa wengine ambao tukiifunga tutakuwa inaharibia watu wengine. Mheshimiwa Spika sioni kuwa itakuwa sawa ingekuwa tunapanda mmea ambao una athari hadi tukauza kwa wale wakulima nyumbani kwao pia nao wangepanya bidii ili ufungwe ama usiletwe katika sehemu hiyo. Kwa hivyo moja kwa moja mimi langu ni kusema kwamba napinga vikali swala la uuzaji na utumiaji wa *Mogokaa* hapa Mombasa na vilevile ninaomba wenzangu tunapokaa na kufikiria maswala haya ni muhimu kutengeza sheria kuhakikisha kwamba huu *Mogokaa* hata kama unasemekana na serikali kuu kwamba si *drug* ili tuweze kupeana njia ya kusumbua uuzaji na utumiaji wa *Mogokaa* ndani ya Mombasa. Unapoenda kule Port Reiz katika Hospitali ya Machizi asilimia 85 ya watu ambao wako pale ni vijana walio athirika na *Mogokaa*.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika swala la *Mogokaa* katika jamii yetu si swala la kuchekea, wala si swala la mzaha, si swala la kuangalia kama ambaye tunalifanyia mchezo. Uchumi wetu unadorora kwa sababu ya swala la *Mogokaa* kwa siku moja ni pesa nyingi zinaenda katika *Mogokaa*. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika langu kubwa ni kusema kuwa ninapinga vikali utumizi, uuzaji na usambazaji ama utumiaji wa *Mogokaa* katika Kaunti yetu ya Mombasa. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Ahsante sana Mheshimiwa Patrick Mbelle. Naam Mheshimiwa Morgan Matsaki, Kiongozi wa upinzani katika Bunge la Mombasa.

The Leader of Minority (Hon. Matsaki): Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ili niweze pia kuchangia hoja hii ama *statement* ambayo imeletwa na Mheshimiwa Baimu. Kwanza wacha nimshukuru Mheshimiwa mwenza kwa kuleta Taarifa hii katika Bunge hili. Kwa kweli naona mengi Waheshimiwa wameyazungumza; hili si jambo jema kamwe, kwanza kuliruhusu katika Kaunti ya Mombasa hii kwamba liwe linauzwa ovyo ovyo! Changizo lango ni kwamba nikiwa kama Mwanachama wa Kamati ya Fedha hili jambo naona tulilijadili kwa muda mrefu sana ambayo kwamba tulisema kwamba angalau tuje na sheria spesheli ambayo sheria yenyewe tuliongeza gari inavyo ingia hapa yale malipo yataonyesha kwamba itawashinda kufanya biashara hapa. Kwa sababu hayo malipo ama bei tuliyoweka katika sheria ni kubwa sana na hiyo ni njia moja wapo tayari tumeamua kupunguza athari kwa vijana wetu hapa Kaunti ya Mombasa. Pili; kwa wale ambao wanakuwa na uwezo kwa sababu huu ni mmea ambao unakuzwa kwa wingi eneo lile huenda wakawa na uwezo wa kuleta; tungependa pia Kaunti hii ya Mombasa ihakikishe inaweka mikakati muafaka kutafuta sehemu kama vile alivyozungumza Mheshimiwa mwenza awali *Miraa* ilikuwa inauzwa tu eneo tofauti. Kwa hivyo hiyo pia iwekwe mikakati hiyo *Mogokaa* wakiweza kulipa hiyo elfu sabini ni pesa ngapi wanapoleta kuwe na sehemu maalum ya kuuzwa kisha iuzwe kwa wakati unaofaa na wale ambao wanahitajika kula pia wawe tunachukua hatua tuangalie ni ki nani. Kwa hivyo mimi pia naunga mkono Mheshimiwa mwenza vile ameleta hoja hii lakini Kaunti ya Mombasa lazima iwe inaweka mikakati muafaka juu ya hili jambo. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Ahsante sana Mheshimiwa Morgan Matsaki. Mheshimiwa Bernard Ogutu, Mwenyekiti wa Kamati ya Afya tafadhali jibu kama uko na jibu la swala hilo ambalo limeletwa likielekezwa kwako.

Hon. Ogutu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza kabisa nimesikia changizo la Waheshimiwa, lawama nyingi likiekewa vijana; na hata Mheshimiwa Spika kuna wamama ambayo pia wanatumia *Mogokaa* na *Miraa* na imewaathiri pakubwa sana nasikia ikiwa walikuwa wanapiga safari mbili wanakwambia sasa wanataka waende safari sita. Mheshimiwa Spika tukiangalia tuangalie...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Mheshimiwa Mwaka?

Hon. Muludonda: Ahsante Mheshimiwa Spika. Ningependa Mheshimiwa Ogutu atueleze safari anasema kuna safari mbili ama moja sijui ni safari ya kwenda wapi?

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Amesema safari sita wewe wajua mbili.

Hon. Muludonda: Atueleezee safari ya kwenda wapi?

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Mheshimiwa Ogutu elezea Mheshimiwa Mwaka hiyo safari ni ya wapi inaanzia wapi ikienda wapi!

Hon. Ogutu: Mheshimiwa Spika ahsante sana. Ni safari ya kwenda mbinguni Mheshimiwa Spika! Mheshimiwa tutahitaji wiki mbili ili tuweze kupata Taarifa ambayo iko kwa undani maanake hili jambo liko *sensitive* na ni lazima tuangalie kwa upana mkubwa sana Mheshimiwa Spika. Ahsante sana.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Kamati ya Afya, japo hiyo safari ya mbinguni ni kama umeanza kutishia Waheshimiwa ila hilo tutalifuatilia baadae. Mheshimiwa Mariam Baimu, *what is your reaction to the time slot of two weeks to get the response to your statement?*

Hon. Baimu: Thank you, Mr. Speaker Sir. I am very comfortable with the duration of two weeks. Thank you, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Thank you so much. Honourable Members, there was a request for Statement which the Chair had ruled because of absence of the one who had requested. That is order number seven; however, because the Honourable Member immediately I had made that decision walked into the Chambers allow me to resign that decision so that we allow him to make his request for the Statement. So, Honourable, sorry, Clerk, please read out the Statement number seven. That is order paper number seven.

REQUEST FOR STATEMENT BY MEMBER OF COUNTY ASSEMBLY FOR BAMBURI WARD
HONOURABLE PATRICK MBELLE ON THE STALLED CONSTRUCTION OF MAJAONI NEW LIFE ROAD AND
KASHANI ROAD

So, Honourable Patrick Mbelle please proceed?

Hon. Mbelle: Thank you Mr. Speaker, and my apologies for not showing up on time as you had instructed earlier. Mr. Speaker Sir, in this day and time, I stand pursuant to Standing Order number 41, section 2, sub section C to request for a Statement from the Chairperson Committee on Transport and Infrastructure on the stalled construction of Majaoni New Life Road and Kashani Road that leads to Kimbunga. Honourable Speaker, the vital infrastructure projects hold the promise of improved connectivity, economic growth and enhanced quality of life for our communities. However, the current state of affairs is far from promising. Mr. Speaker Sir, the delays in completing these roads have undoubtedly caused frustration and inconvenience among the residents who eagerly anticipate for their completion. It is important that we understand the reason behind these delays and take decisive action to ensure that the projects are brought back to track. Mr. Speaker, in the response of the Chairperson of the Committee of Transport and Infrastructure, that Chairperson should inquire and provide;

1. A comprehensive explanation for the stalled progress on both Majaoni New Life Road and Kashani Road that leads to Matangini through Kimbunga;
2. A clear timeline for when these roads will be completed along with the steps being taken to expedite their construction.

Thank you, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Thank you so much, Honourable Patrick Mbelle. Honourable Hassan Mohammed, Chairperson of the Committee on Transport and Infrastructure, the Vice or any Member of that Committee?

Hon. Ogutu: Thank you, Mr. Speaker. We are requesting for two months Mr. Speaker, to bring an elaborate Report to this Honourable House. Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga): Honourable Bernard Ogutu, I hope you have seen the prayers made and the effect of having those roads not completed on time. Honourable Bernard Ogutu, when a matter of such public interest is brought before this House, it is a clear indication there is an outcry from the public and of essence is the fact that this is an institution or an infrastructure that ought to be used by the public. Therefore, your request for two months to respond to such a serious matter is considered serving injustice to the people of Bamburi Ward! As such, I direct that the Committee on Transport to give a response within the next two weeks. Next Order, Clerk?

ADJOURNMENT

Honourable Members, the House stands adjourned until Tuesday, 30th April, 2024 at 10:00a.m. Thank you.

The House rose at 3:08p.m.